

## **Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijiini (MIVARAF)**

Programu hii inagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA).

Lengo la MIVARAF ni kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi endelevu kwa kuwiwezesha kaya za vijijiini kuongeza kipato na usalama wa chakula. Programu hii inatekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Shughuli za Programu ni uendelezaji wa miundombinu na mifumo ya masoko pamoja na uendelezaji wa huduma za kifedha vijijiini.

Utekelezaji wa Programu hii umekuwa wa mafanikio makubwa kwa kuongeza thamani ya mazao, kuwajengea uwezo na kuwaunganisha na masoko na kuwezesha upatikanaji wa huduma za fedha vijijiini.

Aidha, kwa maeneo yanayopitiwa na barabara zilizojengwa na programu hii, shughuli za kiuchumi zimeongezeka na hivyo kuongeza kipato kwa jamii inayozunguka eneo hilo.

Mradi huu unatekelezwa kwa gharama dola za Kimarekani milioni 169.5.